

UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KATIKA NYUGA ZA KIINSIA: HATARI ILIYOPO INAKABILIWA?

Wallace K. Mlaga

Ikisiri

Makala hii inakusudia kubainisha hatari inayozikabili nyuga za kiinsia. Hatari hiyo sio nyingine bali ni nyuga za kiinsia kupoteza umuhimu wake. Miongoni mwa ithibati ya kuwapo kwa hatari hii ni pamoja na idara mbalimbali za nyuga za kiinsia katika vyuo vikuu mbalimbali kufungwa. Aidha, katika nchi zinazoendelea, idadi ya udahili kwa wanafunzi wa nyuga za kiinsia imeshuka sana. Hii ni kutokana na serikali za nchi husika kupunguza au kuondosha kabisa ufadhili kwa wanafunzi hao. Makala imeonesha sababu za nyuga za kiinsia kuonekana kupoteza umuhimu wake kuwa ni pamoja na maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi yaliyosababisha thamani za nyuga kupimwa zaidi kwa faida za kiuchumi. Aidha, makala imeonesha namna ambavyo utetezi unaotolewa na wadau wa nyuga za kiinsia ambavyo umeonekana kutegemea zaidi huruma kuliko kudhihirisha namna ambavyo nyuga za kiinsia bado zina nafasi ya kufanikisha faida za kiuchumi. Hivyo basi, makala imeweka wazi sifa za wafanyakazi, maarifa yatakiwayo, na stadi zinazohitajika katika zama hizi za kidijiti. Hii imefanyika ili kutoa fursa kwa walimu, wataalamu, na wadau wengine wa nyuga za kiinsia, hususani katika vyuo vikuu, wapate nafasi ya kujifanyia tathimini iwapo kweli michakato yao ya ufundishaji na ujifunzaji inakabiliana na hatari hii iliyopo. Mwisho, makala inamalizia kwa kutoa mapendekezo ya nini kinapaswa kufanyika.

Utangulizi

Kwa muda mrefu sasa, nyuga za kiinsia zimeshuhudiwa zikikumbana na changamoto ya kuonekana kuwa hazina umuhimu tena. Hili limedhihirishwa na ufungwaji wa baadhi ya idara za kiinsia katika vyuo vikuu katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea (Ferris, 2011). Aidha, katika nchi zinazoendelea, zikiwamo Tanzania na Rwanda, idara za kiinsia tunaona kuwa bado hazijafungwa lakini huenda idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika programu za kiinsia sio kubwa sana zikilinganishwa na programu zisizokuwa za kiinsia. Hii inatokana na msimamo wa serikali kuhusiana na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaodahiliwa. Vipaumbele vya utoaji mikopo vimewekwa katika baadhi ya programu, hususani za sayansi na elimu.

Wakati hali ikiendelea hivyo, jambo jingine linajitokeza: vyuo vikuu kwa ujumla wake vinajikuta vikikabiliwa na madai ya kwamba haviwasaidii wanafunzi kuhitimu wakiwa na stadi zinazohitajika katika soko la ajira. Hii ni kutokana na zama hizi kutambuliwa kama zama za kidijiti ambazo pia zinamlazimisha muhitimu kuwa na stadi mahsusi ili aweze kustahimili katika dunia yenye ushindani mkubwa (Bates, 2015). Kutokana na nafasi yangu kama mwalimu na mdau wa nyuga za kiinsia, nimepata shuhuda kadhaa za wahitimu wa baadhi ya programu za kiinsia. Wahitimu hawa wanaweka bayana kuwa hawajui wanaweza kufanya nini kutokana na hicho walichosomea. Kwa hakika, ni kama vile wahitimu hao wanajutia uamuzi walioufanya wa kusomea programu hizo za kiinsia. Hii ni licha ya ukweli kuwa changamoto ya ajira inawakumba wahitimu wengi wa vyuo vikuu pasipo kujali programu walizosomea.

Hivyo basi, makala hii inajielekeza katika kuyashughulikia kwa kina masuala haya mawili ili kubainisha hatari inayozikabili nyuga za kiinsia. Aidha, makala inajadili sababu za nyuga za kiinsia kupoteza umuhimu huku ikiweka bayana utetezi unaotolewa na wadau wa nyuga za kiinsia. Kwa kufanya hivi, makala inakusudia kutoa hamasa kwa wadau wa nyuga za kiinsia kufanya tathimini iwapo ufundishaji na ujifunzaji wa nyuga hizi ulivyo sasa unakabiliana na hatari iliyopo.

Tuna maoni kwamba, wataalamu wote katika nyuga za kiinsia wanakubaliana kuwa kuna hatari kubwa inayozikabili nyuga hizi. Inawezekana pakawa na kutofautiana miongoni mwa wataalamu hao juu ya aina ya hatari, chanzo cha hatari, ukubwa wa hatari, na nini kinapaswa kufanyika. Aidha, kutokana na tofauti zilizopo ndani ya nyuga za kiinsia, hatari husika zinaweza kutazamwa kwa namna tofauti. Jambo ambalo tuna uhakika nalo ni kuwa, wataalamu wote katika nyuga hizi wanakubali kuwa nyuga za kiinsia zinakabiliwa na hatari kubwa. Katika sehemu inayofuata, tunabainisha hatari iliyopo.

Ubainishaji wa Hatari Iliyopo katika Nyuga za Kiinsia

Kuna ithibati ya kuwapo kwa hatari katika nyuga za kiinsia ambayo imebainishwa na wataalamu mbalimbali kwa miaka mingi sasa. Ferris (2011:30) anabainisha kuwa:

Tafakuri ya hivi karibuni kuhusu nyuga za kiinsia imethibitisha kwamba kama ilivyo kwa fasihi linganishi, zinakabiliwa na tatizo... Je, mdororo wa kiuchumi wa hivi karibuni unataka kuchanganywa na kile ambacho kilikuwa ni tatizo tayari kwa nyuga za kiinsia, yaani tatizo la kukosa umuhimu kwa nyuga za kiinsia?

Dondoo hili linaweza bayana kwamba kwa muda mrefu, hata kabla ya kuwapo kwa mdororo wa kiuchumi, tayari nyuga za kiinsia zilikuwa tayari zimeanza kutazamwa kama zilizokosa umuhimu.

Ferris (2011) anaendelea kutanabahisha kwamba katika kipindi hiki chote cha nyuga za insia kutazamwa kama zisizokuwa na umuhimu, wadau wa nyuga za kiinsia walijikita kuthibitisha namna ambavyo nyuga za kiinsia zina umuhimu. Walitoa madai ambayo mara nyingi yalikuwa yakichukua mwelekeo wa kutanabaisha na kutangaza thamani iliyopo katika masuala waliyoshughulika nayo ndani ya nyuga za kiinsia (fasihi, historia, sanaa, na falsafa). Aidha, wanainsia kwa muda mrefu waliamini kwamba masomo ya kiinsia kwa hakika hayakuhitaji kuthibitishwa umuhimu wake. Iliaminika kwamba, umuhimu wa insia upo bayana kabisa. Hii ni tofauti na namna watunga sera na wenye mamlaka wanavyolichukulia suala hili.

Weber (2010) kama anavyorejelewa na Ferris (khj), anabainisha kwamba, katika zama hizi, umuhimu (wa kitu) hauangaliwi kwa kuzingatia sitiari za kiuchumi tu bali pia vigezo katili ambavyo navyo ni vya kiuchumi. Hii inamaanisha kwamba, wanainsia wanapaswa nao kudhihirisha umuhimu wa nyuga zao kwa kuegemea katika faida za kiuchumi. Kwa muhtasari, mabadiliko haya ya kuangalia umuhimu wa kitu kiuchumi yanatazamwa kama mhamo wa historia kutoka katika kuegemea utu, kuanza kuegemea siasa, kisha kuanza kuegemea uchumi kama chanzo kikuu cha umuhimu wa nyuga za kiinsia. Hali hii imefanya nyuga za kiinsia kuishia kusubiria huruma. Ni hadi lini nyuga za kiinsia zitaendelea kuwapo kwa kutegemea huruma?

Wakiongelea kuhusu hatari inayoukumba uga wa fasihi linganishi, Dominguez, Saussy, na Villanueva (2015: xvii) wanasisitiza kuwa, hatari hii inapaswa kutazamwa ndani ya hatari inayoogopesha zaidi ya nyuga za kiinsia kwa jumla, na nafasi ya elimu ya kifasihi. Inatanabahishwa kwamba, “Sasa ni wazi kwamba vyuo vikuu vyenye mwelekeo wa Ki-Humboldt na Ki-Kant vinaonekana kufungwa katika sehemu nyingi duniani, huku nafasi yake ikichukuliwa na “vyuo vikuu vya kikampuni.” Hizi ni taasisi za elimu ya juu ambazo zinaendeshwa kwa kuegemea katika kile ambacho waliberali wapya wanaweza kukitaja kuwa ni nyuga zinazoleta faida papo kwa papo. Faida inapaswa kuonekana mara moja. Kutokana na hali hii, tunaambiwa kuwa idara nyingi za fasihi linganishi kama uga mmojawapo wa kiinsia, sasa zimefungwa katika nchi za Marekani na Kanada. Hii ni ithibati tosha ya hatari kubwa inayozikabili nyuga za kiinsia.

Hali hii haijitokezi katika nchi zilizoendelea tu kama Marekani na Canada, bali pia hata katika nchi zinazoendelea. Hili linaweza kubainika sio tu tunapoangalia idadi

ya wanafunzi wanaodahiliwa katika nyuga za kiinsia, bali pia tunapoangalia utayari wa serikali za nchi zinazoendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wanaoenda kujiunga na programu zilizopo katika nyuga za kiinsia, wakilinganishwa na wale waendao kujiunga na programu nyinginezo.

Maana ya Ujifunzaji katika Nyuga za Kiinsia

Pritchard (2009) katika kuitalii dhana ya ujifunzaji, anaeleza kwanza kuwa ujifunzaji sio suala linalopatikana katika mifumo tu ya kielimu. Aidha, ujifunzaji huanza muda mrefu sana kabla hata ya mtu kwenda shuleni. Zaidi ya hivyo, ujifunzaji huu huendelea hata baada ya mtu kumaliza shule. Hii itoshe kuonesha kwamba kuna ujifunzaji rasimi na ujifunzaji usio rasimi. Wakati wote, aina hizi mbili za ujifunzaji huenda sambamba. Anaongeza kuwa, uelewaji wa mchakato wa ujifunzaji ni muhimu kwa walimu wanaokusudia kutengeneza kazi za ujifunzaji ambazo zitakuwa na manufaa ya kufanikisha ujifunzaji muafaka kutokea madarasani. Kwa mtazamo wetu, ujifunzaji muafaka ni ule unaofanikisha kufikiwa kwa malengo ya ujifunzaji. Malengo ya ujifunzaji, pamoja na mambo mengine, huwekwa bayana na fasili ya ujifunzaji inayoshikiliwa. Hivyo, walimu, wakiwamo wale wa nyuga za kiinsia, wanapaswa kufahamu kuwa kuna fasili tofauti kuhusu ujifunzaji. Hivyo, kuna haja ya kushikilia fasili ile ambayo inaendana na mahitaji ya kipindi hiki cha wakati, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya sera za elimu, na mahitaji ya soko la ajira. Hivyo, walimu wanawajibika kuhakikisha kuwa zile fasili muafaka wanazozishikilia wanaziweka vitendoni ndani ya mchakato wa ufundishaji.

Hivyo, Pritchard (2009) anaweka wazi namna ambavyo ujifunzaji hufasiliwa kwa namna tofauti. Miongoni mwa fasili anazozibainisha ni pamoja na: “Ujifunzaji kama mchakato wa kujipatia maarifa zaidi, au ni mchakato wa namna ya kufanya kitu fulani kama vile kuendesha pikipiki.” Kwa mtazamo wetu, hata kama sio kwa umahsusi wa nyuga za kiinsia tu, kwa kiasi kikubwa, ufundishaji uliopo katika nyuga za kiinsia unaongozwa zaidi na mwelekeo wa kuutazama ujifunzaji kama mchakato wa kujipatia maarifa zaidi. Hivyo, malengo ya msingi ya ufundishaji na ujifunzaji ni kuhakikisha wanafunzi wanapata maarifa.

Hadi leo vyuo vikuu vingi hutumia mihutasari ya kozi au nyaraka za ufafanuzi wa kozi au moduli inayoonesha kwa ubayana kabisa kuwa mtaala unaogemea katika maarifa ndio unaoendelea kutekelezwa. Pasipo shaka, imani inayoshikiliwa ni kuwa mwanafunzi akishapata maarifa, tayari ataweza kuyatumia maarifa hayo katika miktadha mbalimbali ya kimaisha. Suala la kuwafundisha wanafunzi namna ya kuyatumia maarifa linatazamwa kama kazi ya msingi ya vyuo vya kati na wala sio vyuo vikuu.

Mara kadhaa, imeelezwa kuwa kazi ya chuo kikuu ni kufundisha kufikiri (Bates, 2015). Licha ya maelezo haya kuwa ni sahihi kabisa, tatizo tunaloliona hapa, maelezo hayo huenda yameishia kupata tafsiri potofu, hivyo kuishia kumaanisha kuwa vyuo vikuu hupaswa kufundisha kiwango cha juu cha kidhahania. Hii husababisha pasipo haja ya kuonesha namna haya yanayofundishwa yanatumika vipi au yana manufaa gani katika maisha ya wanafunzi ya kila siku wakiwa shuleni na baada ya maisha ya shuleni.

Vaughan, Innes, na Garrison (2013) wanatanabahisha kwamba tafakuri tunduizi ndiyo inayotajwa zaidi kama alama kuu ya elimu ya juu. Hii ndiyo sababu anapendekeza dhana mpya ya 'jumuiya ya kiuchuguzi' kama dhana inayobeba kwa ukamilifu zaidi idili ya tajiriba ya elimu ya juu. Hii itawawezesha wadau kutengeneza mazingira kwa ajili ya tafakuri tunduizi, maamuzi ya kutumia akili, na uelewa kupitia ushirikishaji wa jumuiya ya kiuchunguzi. Kwa maneno mengine, jumuiya ya kiuchunguzi ndiyo mbinu inayoleta matumaini zaidi ya uunganishaji wa pamoja wa michakato ya kiakili ya kitafakuri na kibunifu inayojulikana pia kama tafakuri ya ngazi ya juu. Kwa mwelekeo huu, ufanikishaji wa tafakuri ya ngazi ya juu ni kitu kisichokwepeka kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Tunachoona kuwa kinapungua ni pale ufundishaji wa tafakuri unaposhindwa kuhusishwa na hali halisi za kimaisha.

Mabadiliko Muhimu katika Sifa za Wafanyakazi, Maarifa na Stadi katika Zama za Sasa

Bates (2015) anazirejelea zama za sasa kuwa ni zama za kidijiti. Pamoja na mambo mengine, anasisitiza kuwa zama hizi zimefanya sifa za wafanyakazi, aina ya maarifa, na stadi zinazohitajika kwa wahitimu wa vyuo vikuu kubadilika kwa kasi. Aidha, anabainisha kuwa katika zama hizi kuna ongezeko kubwa zaidi la kuhitajika kwa watu wenye kiwango cha juu zaidi cha elimu kuliko katika zama zilizopita. Hii inatokana na kuhitajika zaidi kwa wafanyakazi wenye sifa za kiwango cha juu.

Sifa za Wafanyakazi wa Zama za Kidijiti

Bates (2015) anabainisha sifa bainifu za wafanyakazi wa zama hizi za kidijiti na, hivyo, kutupa nafasi ya kutafakari ufundishaji na ujifunzaji katika nyuga za kiinsia iwapo unakabiliana na hatari iliyopo au la. Sifa za wafanyakazi hawa ni zifuatazo:

Mosi, mara nyingi hufanya kazi katika makampuni madogo. Makampuni haya huwa na watu wasiozidi kumi. Hivyo, kumbe hata katika nchi zinazoendelea, tunapaswa kuendelea kubadili mtazamo wa kufikiria kuwapo kwa viwanda vikubwa sana vinavyotoa ajira. Tunapaswa kujielekeza katika kutoa hamasa ya kuanzisha makampuni haya madogomadogo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi.

Wataalamu wa nyuga za kiinsia lazima pia watoe mchango wao katika kufanikisha hili.

Pili, wafanyakazi hawa, mara nyingine, humiliki biashara zao wenyewe; yaani, wakati mwingine, hujitengenezea ajira zao wao wenyewe. Hizi ni aina za ajira ambazo hazikuwahi kuwapo hadi pale zilipotengenezwa kutokana na hitaji lililopo. Hii inamaanisha kuwa kuna haja ya kuwa na picha kamili ya aina ya kazi zitakazofanywa na wanafunzi wetu pindi watakapohitimu masomo yao. Hivyo, hata aina ya kazi za ujifunzaji zinapaswa kuendana na mazingira watakayokabiliana nayo katika maisha yao ya kila siku.

Tatu, wafanyakazi hawa hufanya kazi za mkataba au hujiajiri wenyewe na, hivyo, hulazimika kubadilisha kazi kutoka kazi moja hadi kazi nyingine. Sifa hii inatupatia picha pia ya aina ya maarifa na ujuzi watakaouhitaji wanafunzi hawa wa nyuga za kiinsia. Kwa hakika, hawapaswi kuwa na maarifa mahsusi tu. Wakiwa na maarifa mahsusi itawawia vigumu kustahimili ushindani wa zama hizi. Aidha, aina ya ujuzi wanaotakiwa kuwa nao sio mahsusi bali wajengewe mazingira yatakayowawezesha kuwa na aina anuai za ujuzi utakaowezesha kustahimili aina ya ushindani uliopo katika zama hizi.

Nne, kazi zao huonekana kubadilika kadri muda unavyopita. Mabadiliko haya hutokana na maendeleo ya soko na teknolojia. Hii inamaanisha kwamba hata maarifa ya msingi katika kazi zao hubadilika kwa kasi sana. Siyo ajabu leo hii katika baadhi ya vyo kuona mkazo unawekwa sana katika kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na uelewa kuhusu stadi ya ujifunzaji wa kudumu. Ujifunzaji haupaswi kuishia chuoni au darasani tu. Wanafunzi wanapaswa kuandaliwa vyema na kujengewa uwezo wa kuendelea kujifunza katika maisha yao yote baada ya kutoka vyuoni.

Tano, wafanyakazi hawa wana werevu wa kidijiti au wana umilisi wa kidijiti. Hii ni kwa kuwa kipengele cha teknolojia ya kidijiti ni muhimu katika ufanikishaji wa kazi zao. Hii inatuonesha namna ambavyo masomo yote katika nyuga za kiinsia yanapaswa kufungamanishwa na teknolojia ya kidijiti. Hakuna haja tena ya umilisi wa teknolojia ya kidijiti kuachwa mikononi mwa somo moja tu, lile la utangulizi wa kompyuta, linalofundishwa kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza. Kila kozi au moduli katika nyuga za kiinsia inapaswa kufungamanishwa vyema na teknolojia ya kidijiti.

Sita, kutokana na wafanyakazi kujiajiri au kufanya kazi katika kampuni ndogondogo, hujikuta wakilazimika kutimiza wajibu tofautitofauti kama vile kutafuta masoko, usanifu, uhasibu, meneja wa biashara, mipango, afisa bajeti,

mtunzaji wa mahesabu, msimamizi wa mradi, na uandishi wa pendekezo la mradi. Jambo la kujiuliza ni kuwa, wataalamu wa nyuga hizi za kiinsia tumefanya ipasavyo kuhakiksha wahitimu wetu wanakuwa na sifa hizi baada ya kuhitimu?

Saba, wafanyakazi hawa hutegemea sana mitandao isiyo rasmi ya kijamii ili kupata biashara, na hata kuepuka kukosa taarifa muhimu kwa ajili ya ustawi wa kazi zao. Nyuga za kiinsia zimeweka kipaumbele katika kuwasaidia wanafunzi wao kuwa na stadi ya kujenga mitandao thabiti ya kijamii? Kila mwalimu wa kozi au moduli ya nyuga za kiinsia kweli anajiona anao wajibu wa kuhakikisha wanafunzi wake wanajua namna ya kutengeneza mitandao ya kijamii kwa ajili ya ustawi wao katika soko la ajira? Je, hivi walimu au wataalamu wenyewe wanayo maarifa hayo ya namna ya kutengeneza mtandao?

Kutokana na sifa za wafanyakazi wa zama za kidijiti, inaonekana ni bayana kuwa sio rahisi kubashiri kwa ubayana nini ambacho wahitimu wa nyuga mbalimbali watakuwa wakifanya miaka kadhaa baada ya kuhitimu. Hii inatoa tahadhari kwa walimu wa nyuga za kiinsia kuepuka kuwafunga wanafunzi katika fikra za aina mahsusi ya kazi wanazoweza kuzifanya hapo baadaye. Wanafunzi wajengewe misingi ya kuwa huru kukabiliana na mabadiliko yanayojitokeza kwa kasi katika soko la ajira. Aidha, walimu na wanafunzi wao wanapaswa kushiriki kubainisha kwa mawanda mapana nini ambacho wanafunzi wanaweza kukifanya kutokana na kile wanachojifunza katika somo, moduli na hata programu husika. Hii ittoa fursa ya kufanya tathimini iwapo wanafunzi husika wana maarifa na stadi za kuwawezesha kufanya hicho wanachofikiri wanaweza kukifanya. Hata tathimini pia inaweza kufanyika kwa kuangalia maendeleo ya wanafunzi iwapo wana maarifa na stadi muhimu zinazohitajika.

Baada ya kuangalia sifa za wafanyakazi wa zama za kidijiti, ni muhimu kufafanua stadi muhimu zinazohitajika katika zama hizi. Hii ittoa nafasi pia kufanya tafakuri juu ya ufundishaji na ujifunzaji katika nyuga za kiinsia iwapo unatilia maanani stadi hizi.

Stadi Muhimu katika Zama za Kidijiti

Bates (2015) anaanza kwa kutueleza kuwa maarifa hujumuisha vipengele viwili vinavyohusiana kwa karibu, lakini ambavyo ni tofauti: maudhui na stadi. Maudhui ni jumla ya ukweli, mawazo, kanuni, ushahidi, ufafanuzi wa michakato, au taratibu. Anapokuja katika suala la stadi, mtaalamu huyu ni kama anasema kuwa, suala la na maudhui ni kitu kimoja na stadi ni kitu kingine. Anaonesha kuwa na mashaka iwapo stadi wanazozipata wanafunzi zinaendana kweli na mahitaji ya zama za sasa za

kidijiti. Kwa maneno mengine, ni kama anauliza, stadi hizi zinawafanya kweli wanafunzi wawe na sifa za wafanyakazi wa zama za kidijiti?

Kwa mtazamo wetu, kwanza tunakubaliana na mtaalamu huyu juu ya haja ya kuwapo kwa muunganiko baina ya maudhui na stadi. Aidha, tunaweza kutazama pia maarifa na stadi kama vitu viwili vinavyotegemeana. Stadi ni utumiaji wa maarifa katika kukabiliana na hali mbalimbali katika maisha. Kwa maneno mengine, stadi ni kujua namna ya kuyatumia maarifa. Hivyo, maarifa sahihi ni msingi wa stadi sahihi. REB (2015) katika mihutisari ya masomo mbalimbali, ikiwamo Kiswahili, inaonesha kwa ubayana namna maarifa na stadi zinavyohusiana kwa ukaribu katika namna ya kutegemeana.

Hivyo, mtu anaweza kuwa na maarifa sahihi lakini asiwe na stadi sahihi. Ili mwanafunzi awe na stadi sahihi, ni lazima awezeshwe kuzijenga stadi hizo sahihi kwa kuzingatia mbinu sahihi za ufundishaji na ujifunzaji. Mtu anaweza kuwa na maarifa mengi, lakini asijue namna ya kuyatumia. Hivyo, walimu na wataalamu katika nyuga za kiinsia tuna changamoto ya kuhakikisha maarifa wanayoyapata wanafunzi wetu ni sahihi na namna wanavyoyapata maarifa hayo ifanikishe kuwasaidia kujenga stadi sahihi zinazohitajika katika zama hizi za kidijiti.

Bodi ya Mikutano ya Canada (2014) kama inavyorejelewa na Bates (2015), inafafanua stadi saba muhimu katika zama hizi za kidijiti. Hii ina maana kwamba maarifa yanapaswa kuendana na stadi hizi saba muhimu katika zama hizi. Tunaona kwamba kuna haja pia ya kuzibainisha na kuzifafanua stadi hizi huku tukizihusisha na tafakari ya ufundishaji na ujifunzaji katika nyuga za kiinsia. Hii itatoa nafasi kwa walimu, wanafunzi, na wadau wengine katika nyuga za kiinsia kutathimini kile wanachokifanya iwapo kinaendana na mahitaji ya zama hizi. Aidha, tafakuri ya stadi hizi itaonesha pia ni kwa namna gani nyuga za kiinsia bado zina nafasi muhimu sana hata katika zama hizi za sasa. Stadi saba zinazoshughulikiwa ni hizi zifuatazo:

Mosi, ni stadi za mawasiliano. Stadi hii ni ya muhimu sana katika kumuwezesha mtu yeyote kustawi katika zama za sasa. Sio ajabu hata katika mihustasari ya masomo yote yanayofundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu nchini Rwanda, stadi hii imetiliwa mkazo. Kila somo limekusudiwa lishiriki ipasavyo katika kufanikisha au kukuza stadi hii miongoni mwa wanafunzi. Stadi za kimawasiliano hapa tunarejea kuanzia zile za kimapokeo kama vile kusoma, kuandika, kusikiliza, na kuzungumza. Kisha stadi za kimawasiliano za kisasa kama vile mawasiliano kupitia mitandao ya kijamii.

Suala la kujiuliza, katika vyuo vyetu, hususani katika programu za kiinsia, kweli tunaweka mkazo wa kutosha katika kufundisha stadi za mawasiliano? Tuna uelewa wa pamoja kuhusu stadi za mawasiliano? Hivi, kila mwalimu katika nyuga za kiinsia anajiona ana wajibu wa kuwasaidia wanafunzi wake kujenga stadi za mawasiliano? Hivi, kozi zetu zote, iwe katika Kiswahili au historia kwa mfano, zimejikita kwa kiasi gani kujenga stadi za mawasiliano kwa wanafunzi wetu? Je, walimu tunaridhika na namna wanafunzi wetu wanavyoandika? Vipi kuhusu namna wanavyozungumza? Vipi kuhusu uwezo wao wa kusikiliza? Hivi, huwa tunawafundisha kuandika kuhusu nini? Hicho wanachoandika ndicho watakachoenda kuandika katika maisha ya baada ya shule?

Kwa upande wa stadi za mawasiliano za mitandao ya kijamii, ni muhimu wanafunzi wetu wakafundishwa hata namna ya kutengeneza video za *Youtube* zinazoonesha kazi anuai za wanafunzi, uwezo wa kuwafikia watu wengi kupitia intaneti, na uanzishaji wa miradi ya kuingiza pesa kupitia mitandao ya kijamii. Pia, wajifunze namna ya kushirikiana kufanya kazi kupitia njia ya mtandao pasipo ulazima wa kukaa mahali pamoja, pamoja na matumizi ya teknolojia na midia mbalimbali kulingana na mahitaji ya taaluma na kazi mahsusi. Kwa mfano, leo mwanafunzi anaweza kuchapisha vitabu vyake mwenyewe kwa njia ya mtandao pasipo kulazimika kulipa pesa yeyote. Je, wanawezeshwa kiasi gani kujifunza haya?

Stadi ya pili inahusiana na uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea. Hii ina maana ya kwamba mwanafunzi anawezeshwa kufikia kiwango cha kuona kuwa ni jukumu lake kushughulika na kile anachotaka kujifunza yeye mwenyewe. Kwamba, ana wajibu wa: kubainisha nini anataka kujua au kujifunza, na ni wapi atayapata hayo maarifa. Hii ni hali atakayoendelea nayo hata kazini. Kwani, kila wakati atalazimika kujifunza mambo mapya kutokana na namna maarifa mapya yanavyoibuka kila siku.

Mabadiliko ya kazini yanaweza kuwa ni pamoja na zana mpya, namna mpya ya ufanyaji kazi, au kujifunza juu ya watu wepi unaohitaji kuwafahamu ili kuikamilisha kazi. Hii ina maana kwamba, mwanafunzi akifanywa kuwa tegemezi sana kwa mwalimu, itamuathiri hata katika maisha yake ya baada ya shuleni. Mwanafunzi wa namna hii hatakuwa na umiliki wa ujifunzaji. Ili suala hili lifanikiwe, mitazamo ya walimu pia inapaswa kubadilika. Mwalimu hapaswi kujiona kuwa yeye ndiye mmiliki wa maarifa na wanafunzi ni wapokeaji tu. Mabadiliko ya kimtazamo yanapaswa kuendana pia na mabadiliko ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Ndipo palipo na haja pia hata ya walimu wa nyuga za kiinsia kuzifahamu nadharia za kisasa za ujifunzaji.

Tatu ni kuhusiana na itikeli na uwajibikaji. Kwa uzoefu wetu, kati ya mambo ambayo yanapigiwa kelele siku hizi ni kukosekana kwa vijana waaminifu. Watu wengi wanatafuta watu wa kufanya nao kazi, lakini kila wakiangalia hawawapati vijana wenye sifa. Sio kwa kuwa vijana wanaotafutwa ni wenye maarifa au stadi fulani mahsusi kiasi cha kufanya iwe vigumu kuwapata. Vijana wenye maarifa na stadi mahsusi wanaweza kuwapo kabisa lakini wakakosa kusimama katika misingi ya kiitikeli na kiuwajibikaji. Ni muhimu walimu na wataalamu wa nyuga za kiinsia tujiulize tunashiriki kwa kiwango gani katika kuhakikisha wanafunzi wetu wanaiva katika misingi ya kiitikeli na kiuwajibikaji. Tunawasaidia wanafunzi waone fahari kubwa katika kuwajibika kwa ukamilifu katika kutimiza majukumu yao mbalimbali huku wakiendana na misingi ya kiitikeli ya kazi au majukumu wanayoyatekeleza? Walimu wote katika nyuga za kiinsia wanajua kuwa huu ni wajibu wao muhimu? Ni mikakati ipi inayotumiwa kufanikisha itikeli na uwajibikaji miongoni mwa wanafunzi? Umuhimu wa suala hili umeifanya Serikali ya Rwanda, kupitia Bodi ya Elimu Rwanda, kuweka kipengele cha thamani na mitazamo inayopaswa kupandikizwa miongoni mwa wanafunzi wa ngazi zote za elimu. Licha ya kusudio hili la serikali, huko madarasani utekelezaji upo namna gani?

Stadi ya nne ni ushirikiano wa kitimu na unyumbulifu. Licha ya wafanyakazi wa zama za kidijiti kufanya kazi kwa kujitegemea au katika kampuni ndogo, kwa hakika, wafanyakazi hawa hutegemea sana ushirikiano. Hivyo, wafanyakazi wa zama hizi wanapaswa kujua namna ya kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na wenzake, wateja, na hata washirika kwa njia ya mtandao. Ili kufanikisha utekelezaji wa kazi yoyote au utatuzi wa tatizo, huhitajika sana ushirikiano wa kitimu na unyumbulifu kwa ajili ya mafanikio ya kampuni. Hivyo, ni muhimu walimu na wataalamu wa nyuga za kiinsia kujiuliza iwapo wamefanikisha kwa kiasi gani wanafunzi wao kuwa na ushirikiano wa kitimu na unyumbulifu unaohitajika kufanikisha miradi mbalimbali.

Tano, ni stadi ya tafakuri. Stadi hii inahusisha stadi ndogondogo kama vile tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatizo, tafakuri bunifu, uletaji wa upya au uasili, na upangaji wa mikakati. Inaelezwa pia kwamba, kati ya stadi zote zinazohitajika katika zama hizi za kidijiti, stadi za tafakuri ni miongoni mwa stadi muhimu zaidi. Miongoni mwa sababu za stadi hii kuwa na umuhimu ni kwa kuwa biashara leo hii zinategemea kustawi sana kutokana na uanzishwaji wa bidhaa mpya, huduma mpya, michakato mipya ya kupunguza gharama, huku ikiongeza fursa ya kiushindani. Je, programu zinazohusiana na nyuga za kiinsia katika vyuo vyetu mbalimbali zinafundisha stadi hizi za tafakuri? Ufundishaji huo unazihusisha stadi hizi na maisha halisi ya kila siku? Ufundishaji huo hauishii tu kwenye mawanda ya kidhahania? Hivi kila mwalimu wa kozi au moduli katika nyuga za kiinsia anajua

kwa dhati kuwa anahusika na kuikuza stadi hii ya tafakuri miongoni mwa wanafunzi wake? Kwanza, wote wana uelewa wa kutosha kuhusu stadi za tafakuri? Kila mmoja ana mikakati muafaka ya kuzikuza stadi hizi za tafakuri?

Stadi ya sita ni ya kidijiti. Hii ni stadi muhimu kwa kuwa zama hizi zinategemea sana matumizi ya teknolojia. Jambo la muhimu hapa ni kuwa stadi hii ni lazima iambatanishwe na maarifa ya uga mahsusi. Kama ni kwa mwanafunzi wa Kiswahili, anafundishwa namna ya kutumia teknolojia katika kufundisha lugha kwa wageni? Amefundishwa teknolojia za uandishi na uchapishaji? Amefundishwa teknolojia mbalimbali zitakazomuwezesha kujiajiri au kutengeneza ajira katika uga aliosomea? Hii ina maana sio tu kuishia kufundisha matumizi ya teknolojia kijumla sana. Hapa ndipo wengi huenda huwa wanafikiri ile kozi au moduli ya utangulizi wa kompyuta ndio kozi au moduli pekee inayomuwezesha mwanafunzi kupata stadi za kidijiti. Ni muhimu kila mwanafunzi wa moduli yoyote katika nyuga za kiinsia kuchukua jukumu la kukuza stadi za kidijiti miongoni mwa wanafunzi.

Stadi ya saba ni menejimenti ya maarifa. Kama tulivyokwisha kuona, maarifa sio tu kuwa yanabadilika kwa kasi sana kutokana na tafiti mpya, maendeleo mapya, na usambazaji wa kazi wa mawazo, na utendaji kupitia mtandao bali pia vyanzo vya maarifa vinaongezeka huku vikitofautiana juu ya uthabiti au uhalali wa taarifa. Hivyo, maarifa anayojifunza mtu katika taaluma yoyote kutoka chuo kikuu yanaweza kupoteza maana ndani ya muda mfupi. Kuna maarifa mengi kiasi kwamba sio rahisi mtu kuwa na ujuzi wa maarifa hayo yote hata kama angesoma programu moja kwa miaka kumi. Hivyo, katika mazingira kama haya, stadi muhimu inakuwa menejimenti ya maarifa. Ikiwa na maana ya namna ya kutafuta, kuchambua, kutathimini, kutumia, na kusambaza taarifa ndani ya muktadha maalumu. Stadi hii nayo inaweza kufanikishwa pale tu ambapo walimu na wanafunzi watakubali kubadilisha mitazamo yao. Mwalimu akubali kumfanya mwanafunzi kuwajibika zaidi katika ujifunzaji wake kwa kumuandalia kazi muafaka za ujifunzaji. Mwanafunzi naye anapoandaliwa kazi muafaka za ujifunzaji asione kuwa mwalimu anamuelemea. Aelewe kwa nini ametakiwa kujifunza kwa namna hiyo badala ya njia ile tu ya kupewa notisi na mwalimu.

Maarifa katika Zama za Kidijiti: Maarifa ni Bidhaa

Gilbert (2005) kama anavyorejelewa na Bates (2015) anatanabahisha kwamba, katika zama za kidijiti, maarifa mapya yanahusu ubidhaishaji wa maarifa. Hivyo, maarifa hufasiliwa sio kupitia maana yake bali kupitia nini kinaweza kufanyika kupitia maarifa hayo. Hivyo, uwezo wa kumiliki, kununua, na kuuza maarifa umechangia kwa namna nyingi maendeleo ya jamii hii mpya ya kidijiti.

Katika jamii ya kidijiti, mkazo unawekwa katika utumizi wa maarifa kwa malengo ya kibiashara. Matokeo yake ni kuweka upendeleo zaidi katika aina fulani ya maarifa, hususani yale yanayoleta matokeo ya kivitendo ndani ya muda mfupi kuliko yale maarifa ya kiutafiti yanayoleta matokeo baada ya muda mrefu. Swala la kujiuliza ni kwamba, walimu na wataalamu wote katika nyuga za kiinsia wanajua kuwa ni aina ipi ya maarifa inayohitajika zaidi? Je, wao kama wataalamu wameweka mkazo katika aina ipi ya maarifa? Wanafunzi wanajifunza kwa namna gani kuyapata hayo maarifa na namna ya kuyatumia? Wahadhiri, walimu na wakufunzi wanajua kwa ukamilifu kwamba maarifa hayo yanaweza kufanywa kuwa tumizi kwa namna gani? Wameonesha mfano kwa vitendo namna ya kuyatumia hayo maarifa na kuleta manufaa yanayoonekana katika jamii? Kwa nini walimu waendeleo kuwaeleza wanafunzi kinadharia tu namna ya kuyatumia hayo maarifa badala ya kuwaonesha kwa mifano inayoshikika na kuonekana?

Licha ya Bates (2015) kuonesha kuwa maarifa ya kitaaluma ni msingi wa maarifa tumizi, tuna mtazamo kuwa huenda katika nyuga nyingi za kiinsia, mkazo umewekwa zaidi katika ufundishaji wa maarifa ya kitaaluma kuliko maarifa tumizi. Ni kama vile walimu wanaamini kwamba mwanafunzi anapofundishwa tu maarifa yale ya kitaaluma tayari hapohapo anakuwa pia amefanikiwa kupata maarifa tumizi.

Katika jamii ya kidijiti, kuna mwelekeo wa kutenganisha maarifa tumizi na maarifa ya kitaaluma. Maarifa yanayosababisha ubunifu na shughuli za kibiashara ndiyo hutazamwa kama uti wa mgongo wa maendeleo ya kiuchumi. Gilbert (2005) kama anavyorejelewa na Bates (2015) anabainisha kwamba katika jamii ya kidijiti, kumekuwa na mwelekeo wa kuweka thamani zaidi katika maarifa tumizi kuliko maarifa ya kitaaluma, huku vyuo vikuu vikiwa na mtazamo tofauti.

Bates (2015) anamtazama Gilbert (2005) kama mwenye mtazamo wa kwamba maarifa tumizi ni kujua namna ya kufanya vitu, na hivyo kuyafanya maarifa haya kuwa na sifa ya kuegemezwa katika maingiliano ya nyuga. Kwa hakika, iwapo tutahitaji wanafunzi wetu waweze kuwa na maarifa yanayowawezesha kutenda katika miktadha tofauti, hatuna budi kukumbatia mkabala wa maingiliano ya nyuga. Hatuna tena sababu ya kujikita kutafuta upekee au umahsusni wa somo au uga fulani.

Mwelekeo wa Gilbert (2005) kuhusu kutengenisha maarifa ya kitaaluma dhidi ya maarifa mengine una dosari kwa kueleza kuwa, maarifa ya kitaaluma hayawezi kuwa sahihi. Pamoja na hivyo, unaeleza changamoto iliyopo katika masomo au programu kadhaa katika nyuga za kiinsia. Hii huweza kutokana na ufundishaji na ujifunzaji unavyofanyika. Kile kinachofundishwa huwa hakihusishwi na namna kinavyoweza kutumika kwa manufaa ya jamii. Hivyo, kuna haja ya wadau katika nyuga za kiinsia kuweka bayana maarifa yote tumizi wanavyoweza kuyafundisha.

Pia, maarifa ya kitaaluma wanayoyafundisha yanapaswa pia kuoneshwa namna gani yanaweza kutumika. Wanafunzi wapewe mazoezi muafaka ya kuwawezesha kuyatumia maarifa ya kitaaluma katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha yao.

Hitimisho

Ili kuikabili kwa dhati hatari inayozikabili nyuga mbalimbali za kiinsia, kuna haja ya kuzingatia yafuatayo: Mosi, kuna haja ya kuufumbata ipasavyo mkabala wa maingiliano ya nyuga. Hakuna tena sababu kwa kila uga kujikita kutafuta umahsusi au upekee wake ili kujihalalisha. Pili, walimu na wanafunzi wa nyuga za kiinsia wanapaswa kuelekeza nguvu zao katika ufundishaji na ujifunzaji wa maarifa na stadi zinazoendana na zama hizi za kidijiti. Tatu, kuna haja ya walimu wa nyuga za kiinsia kuona umuhimu wa kujifunza nadharia za ujifunzaji zinazopigiwa chapuo katika zama za sasa. Hii itawasaidia sana hata katika kufanya tathimini ya namna wanavyoweza ujifunzaji kwa wanafunzi wao, hivyo kufanya maamuzi sahihi juu ya nini wanapaswa kufanya. Nne, kuna haja ya walimu pia kuweka kusudio la kujifunza juu ya aina mbalimbali ya mitaala, hivyo kuwa katika nafasi siyo tu ya kutengeneza programu zinazoendana na mahitaji, lakini pia kuzitekeleza programu hizo kwa usahihi. Tano, walimu na wanafunzi wanapaswa kukubali kubadilisha mitazamo yao kuhusu ufundishaji na ujifunzaji. Zama za mwalimu kujiona kuwa chanzo cha maarifa zimepitwa na wakati. Mwalimu ajitambue kuwa yeye ni mwezeshaji na hivyo ana wajibu wa kutengeneza kazi muafaka za ujifunzaji. Aidha, wanafunzi nao waachane na tabia ya kumtegemea mwalimu kama chanzo pekee cha maarifa. Huenda wanafunzi hufanya hivi kutokana na unafuu wanaoupata katika kufika mwisho wa kozi au moduli husika na sio katika unafuu wa ujifunzaji. Kwani, mwalimu huwapatia notisi na wao kazi yao huwa ni kuzikariri. Kukariri huwa sio kujifunza. Mwanafunzi lazima ashiriki kikamilifu katika kuyatengeneza maarifa.

Marejeleo

- Bates. A.W. (2015). *Teaching in Digital Ages: Guidelines for Designing Teaching and Learning*. Vancouver: Tony Bates Associates LTD.
- Dominguez, C., Saussy, H., na Villanueva, D. (2015). *Introducing Comparative Literature: New Trends and Applications*. London, New York: Routledge
- Ferris, D. (2011). “Why Compare” in *A Companion to Comparative Literature* by Behdad, A. & Thomas, D. (eds.). Sussex: Wiley- Blackwell
- Pritchard, A. (2009). *Ways of Learning: Learning Theories and Learning Styles in the Classroom*. London, New York: Routledge.
- REB (2015). *Muhtasari wa Somo la Kiswahili Kidato 4 - 6: Mchepuo wa Lugha*. Kigali: REB.

Vaughan, D. N., Innes, C. M., na Garrison, R. D. (2013). *Teaching in Blended Learning Environments: Creating and Sustaining Communities of Inquiry*. Edmonton: AU PRESS.